

## KISWAHILI

Tarehe: 14/Juni/2024

Wakati: 8h30'-11h30'



# MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA TATU

**KIWANGO:**

Kidato cha tano

**MICHEPUO**

LFK

**MUDA:**

Masaa matatu (3)

**ALAMA:**

..... / 100

CAMIS:

..... / 60

## MAELEKEZO

- Usifungue karatasi hii ya mtihani bila ruhusa.
- Mtihani huu unaundwa na sehemu kuu nne:
  - Ufahamu (alama 30),
  - Sarufi na Matumizi ya Lugha (alama 30),
  - Fasihi (alama 25),
  - Utungaji (alama 15).
- Mtihani huu unaundwa na maswali 23.
- Jibu maswali yote kulingana na maelekezo yaliyotolewa.
- Tumia kalamu ya bluu au kalamu nyeusi

**Soma kifungu cha habari kinachofuata, kisha jibu maswali yaliyoulizwa juu yake.**

**Usafi wa mwili**

Usafi wa mwili ni miongoni mwa mambo ambayo binadamu analazimishwa kutilia mkazo sana. Msisitizo huu unatokana na kuwa usafi wa mwili una uhusiano wa karibu sana na uboreshaji wa afya yetu.

Usafi kama hali ya kutokuwa na uchafu, unaweza kuhusu: Mazingira yetu (kama vile usafi wa nyumba); vitu tunavyotumia katika kazi mbalimbali (kama vile usafi wa vyombo vya jikoni); Luga tunavyotumia (kama vile usafi wa lugha au maneno); Roho zetu (kama vile usafi wa roho yaani kutakasa roho zetu kutokana na sala); Mwili wetu (Mfano: Usafi wa meno) na kadhalika.

Ila, katika kifungu cha habari hiki, tutazungumzia usafi wa mwili tu.

Wazazi na walezi wana nafasi kuu na muhimu katika makuzi na usafi wa mwili wa mtoto. Kitendo cha kumfunza mtoto kuhusu usafi wa mwili ni njia bora kabisa ya kumwepusha na maadhara mengi. Mtoto anavyokua ndivyo azoeavyo. Misingi sahihi ya usafi anayofundishwa na watu hao ndiyo inayomwezesha kutilia mkazo usafi wa mwili wake katika maisha yake ya baadaye. Misingi ya usafi wa mwili inapaswa kufundishwa na kuwa sehemu moja ya maisha ya kila siku ya binadamu. Usafi wa mwili unawahu su watu wote, awe: Mtoto wa shule za chekechea; Mtoto wa shule za msingi; Mtoto wa shule za sekondari; Mwanafunzi wa vyuo vikuu; Wafanyakazi wote; Watu wote wanaohitaji kuboresha afya yao.

Mambo ya kuzingatia katika usafi wa mwili ni mengi lakini yaliyo muhimu sana ni yale yanayohusu: Usafi wa kinywa; Usafi wa mikono; Usafi wa nywele; Usafi wa nguo.

Kuhusu usafi wa kinywa, madhara yanayoweza kusababishwa na uchafu wa sehemu hizo ni mengi. Meno machafu huweza kuoza na kuvunjika, fizi inaweza kuvimba, kuoza na kutoa harufu mbaya na kadhalika. Upigaji mswaki wa mara kwa mara unashauriwa kwa watu wote. Mtu huweza kupiga mswaki: Asubuhi anapoamka kabla ya kifunguakinywa; Kila mara baada ya chakula hasa vyakula vyenye sukari; Usiku kabla ya kulala.

Vyakula vyenye sukari husababisha ugonjwa wa kuoza kwa meno kwa kiwango cha juu. Usafi wa mikono nao unapaswa kuzingatiwa sana. Uchafu wa mikono unaweza kusababisha magonjwa mbalimbali kama vile kuharisha, kipindupindu, kuhara damu, nimonia, ebola na mengineyo ambayo kila mwaka husababisha vifo vya watu wengi sana. Njia moja bora ya kujikinga na magonjwa na kuepuka kueneza magonjwa ni “kunawa au kuosha mikono kwa ukawaida”. Ni rahisi kupata homa na mafua kama utagusa pua au macho yako huku mikono yako ikiwa na viini.

Pindi unataka kulinda afya yako na ya wengine dhidi ya maambukizo ya magonjwa, unapaswa kunawa mikono: Baada ya kutoka chooni; Kabla ya kutayarisha, kuhudumia au kula chakula; Baada ya kupiga chafya, kukohoa au kupenga kamasi; Baada ya kutupa takataka; Kabla na baada ya kumtembelea mgonjwa; Baada ya kumgusa mnyama au kinyasi cha mnyama; Baada ya kumbadilishia nepi mtoto au kumsaidia kutumia choo; Kabla na baada ya kutibu jeraha au kidonda na kadhalika.

Kunawa au kuosha mikono hufanyika namna gani? Hizi zifuatazi ni hatua za kufuatalia ili kitendo hicho kifanyike ipaswavyo: Lowesha mikono yako katika maji safi ya bomba na kisha utumie sabuni; Sugua mikono yako pamoja ili kupata povu. Usisahau kusafisha kucha, vidole, pande zote za mkono na katikati mwa vidole vyako; Endelea kusugua kwa sekunde ishirini (20) hivi; Safisha mikono yako katika maji safi yanayotiririka; Kausha mikono yako kwa kutumia kitambaa safi au karatsi ya kukaushia mikono.

Kuhusu kucha, hakikisha kuwa zimekatwa ili viini nya maradhi visije vikajificha chini ya kucha. Ni rahisi kufanya hivyo ili kuzuia magonjwa na kuokoa maisha yako.

Kuhusu usafi wa nywele, zinaweza kukatwa au kusukwa mara kwa mara na kusafishwa vizuri kwa kutumia maji na sabuni. Kitendo hiki kitasaidia katika kupunguza uyabisi na kuzuia chawa wa kichwani iwapo nywele zitakuwa chafu na kutooshwa vizuri.

Usafi wa mwili unahusiana sana na usafi wa nguo. Ni lazima wakati wowote nguo zetu ziwe safi yaani zifuliwe kwa sabuni na zibadilishwe mara kwa mara ili mtu asiwe na mwenendo wa kihuni.

Nguo zinazohusika ni: Mavazi ya nje kama vile shati, mpira, blauzi, kofia, kanzu, viatu, suruali...; Mavazi ya ndani kama vile chupi, soksi, sindiria,...; Mashuka kitandani na taulo. Soksi, taulo, mashuka au sindiria zikivaliwa kwa muda mrefu bila kubadilishwa hutoa harufu mbaya. Hivyo, chawa nao huweza kujitokeza na kuyahatarisha maisha yako.

Dumisha usafi wa mwili ili uweze kujilinda na maambukizi ya maradhi na kuepusha kuenea kwake. Kumbuka kuwa “Kinga ni bora kuliko tiba”.

### **Maswali ya ufahamu**

- 1)** Yataje mambo manne yanayoweza kuhusika na usafi. **(Alama 2)**
- 2)** Je, ni upi umuhimu wa kumfunza mtoto kuhusu usafi wa mwili? **(Alama 3)**
- 3)** “Baadhi ya watu hawana budi kutohusika na usafi wa mwili”. Eleza waziwazi. **(Alama 2)**
- 4)** Eleza tofauti baina ya “shule za chekechea” na “shule za msingi”. **(Alama 4)**
- 5)** Kwa nini usafi wa kinywa ni muhimu sana? Eleza. **(Alama 3)**
- 6)** Ni wakati gani tunatakiwa kusugua meno? **(Alama 2)**

- 7)** Ni wakati gani tunalazimishwa kunawa mikono yetu? **(Alama 2)**
- 8)** Namna gani kitendo cha kuosha mikono kinafanyika? **(Alama 2)**
- 9)** Kwa nini ni lazima nguo za ndani za mtu ziwe safi? **(Alama 3)**
- 10)** Baada ya kusoma kisa hiki, fupisha habari nzima katika maneno 50. **(Alama 4)**
- 11)** Tumia maneno yafuatayo kutoka kifungu cha habari ulichopewa, kuunda sentensi yenyе maana. **(Alama 3)**
- a)** Meno
  - b)** Mikono
  - c)** kucha

#### **SEHEMU YA II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama 30)**

- 12)** Kamilisha ipaswavyo sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo: ***elimu, mikakati, uhaba.*** **(Alama 3)**
- a) Ni lazima serikali yetu iunde ..... thabiti ya kufundisha fasihi simulizi shulenii.
  - b) Uvumbuzi wa maandishi ni mojawapo kati ya mambo yanayosababisha ..... wa kazi za fasihi simulizi.
  - c) Serikali ya Rwanda imepiga hatua kubwa katika kuendeleza ..... isiyo na ubaguzi.
- 13)** Tumia vitenzi vifuatavyo ujaze tungo za masharti zinazofuata ili ziwe na maana kamili: (**kuwa, kupata, kuchanjwa, kujenga, kujuua**) **(Alama 5)**
- a) ..... na pesa, ningenunua mbolea ili kurutubisha shamba langu na kupata mavuno mengi.
  - b) Nisingewafuga ng'ombe wengi, ..... maziwa ya kutosha.
  - c) Ningalijua, ..... ili kujikinga na ugonjwa wa kifua kikuu.
  - d) Ningalikuwa na pesa, ..... nyuma ya kifahari Jijini Kigali.
  - e) ..... wakati anapopatikana, ningelikwenda kumwona daktari wa meno.
- 14)** Changanua tungo uliyopewa hapa chini kwa njia ya visanduku. **(Alama 3)**

Shangazi yangu na mjomba walisema ukweli.

**15)** Katika uandishi wa matangazo mambo mengi yanazingatiwa.

Tumia **NDIYO** kwa jibu lililo sahihi na **HAPANA** kwa jibu lisilo sahihi.

**(Alama 5)**

- a) Kuandika kichwa cha tangazo.
- b) Kumbukumbu namba (ikiwa unayo).
- c) Kutaja mtu au shirika linalotangaza.
- d) Salaam.
- e) Kuonyesha anwani ya mtoa tangazo.

**16)** Andika kwa upya sentensi zifuatazo kutokana na maelezo

uliyopewa katika mabano. **(Alama 10)**

- a) Kabanda alirutubisha shamba ili kupata mavuno mengi. (Wakati ujao, hali yakinishi)
- b) Mariamu alisamehe watu wote waliopora mali yake. (Wakati uliopo, hali kanushi)
- c) Watu wengi hupenda kuomba Mungu kila siku. (Wakati uliopo, hali yakinishi)
- d) Kituo chetu kisingalilenga kutetea haki za watoto, kisingalipiga marufuku ubakaji wa watoto nchini mwetu. (Masharti, hali yakinishi)
- e) Usipomwadhibu mtoto, hatakuwa na nidhamu wala mwenendo bora. (Masharti, hali yakinishi)

**17)** “Barua ni nusu ya kuonana. Thibitisha kauli hii. **(Alama 4)**

### **SEHEMU YA III: FASIHI**

**(Alama 25)**

**18)** Fasihi ina uhusiano wa karibu na lugha pamoja na jamii ya watu. Thibitisha kauli hii. **(Alama 5)**

**19)** “Fasihi simulizi ya Kiswahili ilikuwepo kabla ya majilio ya wageni sehemu za pwani ya Bahari ya Hindi.” Fafanua kauli hii. **(Alama 5)**

**20)** Chagua maana iliyo sawa inayofanana na methali zifuatazo:

**(Alama 6)**

- a) Dawa haitolewi kwa bure:
  - i) Dawa hununuliwa kwenye kituo cha hospitali
  - ii) Dawa za bure hazitibu maradhi
  - iii) Dunia si dunia ya vitu vya bure, nafaa mtu afanye kazi
  - iv) Majibu yote ni sahihi
  
- b) Chovya chovya humaliza buyu la asali.
  - i) Asali iliyo katika buyu huwa na utamu sana.
  - ii) Tunapotenga kitu kwa manufaa ya baadaye (akiba) na kuanza kukimega kidogo kidogo, mwisho tutashtuka tumekimaliza.
  - iii) Tunapotenga kitu kwa manufaa ya baadaye (akiba) na kuanza kukimega kidogo kidogo, mwisho tutapata vitu vingine.
  - iv) Hakuna jibu sahihi.
  
- c) Nguo za kuazima hazisitiri matako.
  - i) Nguo uliyoazima inapendeza sana.
  - ii) Usiwategemee wengine katika kukidhi mahitaji yako.
  - iii) Tegemea watu wengine watakusaidia kutatua matatizo yako.
  - iv) Majibu yote ni sahihi.

**21)** Andika kwa mtindo wa kinathari wazo kuu linalozungumziwa katika ubeti wa kwanza wa shairi lifuatalo: **(Alama 5)**

#### **ASIYESIKIA LA MKUU**

1. Ulevi kitu kibaya, sahibu na kueleza,  
Utakuletea dhiya, kuonyesha miujiza,  
Waja kukuona mbaya, na wao watakubeza,  
Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu.
  
2. Mwisho utafirisika, ponda malikufa kwaja,  
Huja we ukashituka, ukabakia kiwanja,

Pesa zimekuponyoka, zikienda kwa wajanja,  
Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu.

- 22)** Kuna mafunzo na maadili yanayofuatiliwa na jamii kutoka katika  
hadithi ya fasihi simulizi. Thibitisha kauli hii. **(Alama 4)**

**SEHEMU YA IV: UTUNGAJI** **(Alama 15)**

- 23)** Chagua mada moja kati ya hizi zifuatazo kisha utunge insha  
yenye maneno kati ya 150 na 250.  
a) Maneno matamu humtoa nyoka  
pangoni. b) John alipigwa marufuku  
shuleni.

**Mwisho.**

## KISWAHILI

Tarehe: 14/Juni/2024

Wakati: 8h30'-11h30'



# MWONGOZO WA KUKOSOA MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA TATU

KIWANGO:

Kidato cha tano

MICHEPUO

LFK

MUDA:

Saa tatu (3)

ALAMA:

..... / 100

CAMIS:

..... / 60

## MAELEKEZO

- Usifungue karatasi hii ya mtihani bila ruhusa.
- Mtihani huu unaundwa na sehemu kuu nne: Ufahamu, Sarufi na Matumizi ya Lugha, Fasihi na Utungaji.
- Mtihani huu unaundwa na maswali 23.
- Jibu maswali yote kulingana na maelekezo yaliyotolewa.
- Tumia kalamu ya bluu au kalamu nyeusi

**Soma kifungu cha habari kinachofuata, kisha jibu maswali yaliyoulizwa juu yake.**

### **Usafi wa mwili**

Usafi wa mwili ni miogoni mwa mambo ambayo binadamu analazimishwa kutilia mkazo sana. Msisitizo huu unatokana na kuwa usafi wa mwili una uhusiano wa karibu sana na uboreshaji wa afya yetu.

Usafi kama hali ya kutokuwa na uchafu, unaweza kuhusu: Mazingira yetu (kama vile usafi wa nyumba); Vitu tunavyotumia katika kazi mbalimbali (kama vile usafi wa vyombo vya jikoni); Lugha tunayotumia (kama vile usafi wa lugha au maneno); Roho zetu (kama vile usafi wa roho yaani kutakasa roho zetu kutokana na sala); Mwili wetu (Mfano: Usafi wa meno) na kadhalika.

Ila, katika kifungu cha habari hiki, tutazungumzia usafi wa mwili tu.

Wazazi na walezi wana nafasi kuu na muhimu katika makuzi na usafi wa mwili wa mtoto. Kitendo cha kumfunza mtoto kuhusu usafi wa mwili ni njia bora kabisa ya kumwepusha na maadhara mengi. Mtoto anavyokua ndivyo azoeavyo. Misingi sahihi ya usafi anayofundishwa na watu hao ndiyo inayomwezesha kutilia mkazo usafi wa mwili wake katika maisha yake ya baadaye. Misingi ya usafi wa mwili inapaswa kufundishwa na kuwa sehemu moja ya maisha ya kila siku ya binadamu. Usafi wa mwili unawahu su watu wote, awe: Mtoto wa shule za chekechea; Mtoto wa shule za msingi; Mtoto wa shule za sekondari; Mwanafunzi wa vyuo vikuu; Wafanyakazi wote; Watu wote wanaohitaji kuboresha afya yao.

Mambo ya kuzingatia katika usafi wa mwili ni mengi lakini yaliyo muhimu sana ni yale yanayohusu: Usafi wa kinywa; Usafi wa mikono; Usafi wa nywele; Usafi wa nguo.

Kuhusu usafi wa kinywa, madhara yanayoweza kusababishwa na uchafu wa sehemu hizo ni mengi. Meno machafu huweza kuoza na kuvunjika, fizi inaweza kuvimba, kuoza na kutoa harufu mbaya na kadhalika. Upigaji mswaki wa mara kwa mara unashauriwa kwa watu wote. Mtu huweza kupiga mswaki: Asubuhi anapoamka kabla ya kifunguakinywa; Kila mara baada ya chakula hasa vyakula vyenye sukari; Usiku kabla ya kulala.

Vyakula vyenye sukari husababisha ugonjwa wa kuoza kwa meno kwa kiwango cha juu. Usafi wa mikono nao unapaswa kuzingatiwa sana. Uchafu wa mikono unaweza kusababisha magonjwa mbalimbali kama vile kuharisha, kipindupindu, kuhara damu, nimonia, ebola na mengineyo ambayo kila mwaka husababisha vifo vya watu wengi sana. Njia moja bora ya kujikinga na magonjwa na kuepuka kueneza magonjwa ni “kunawa au kuosha mikono kwa ukawaida”. Ni rahisi kupata homa na mafua kama utagusa pua au macho yako huku mikono yako ikiwa na viini.

Pindi unataka kulinda afya yako na ya wengine dhidi ya maambukizo ya magonjwa, unapaswa kunawa mikono: Baada ya kutoka chooni; Kabla ya kutayarisha, kuhudumia au kula chakula; Baada ya kupiga chafya, kukohoa au kupenga kamasi; Baada ya kutupa takataka; Kabla na baada ya kumtembelea mgonjwa; Baada ya kumgusa mnyama au kinyasi cha mnyama; Baada ya kumbadilishia nepi mtoto au kumsaidia kutumia choo; Kabla na baada ya kutibu jeraha au kidonda na kadhalika.

Kunawa au kuosha mikono hufanyika namna gani? Hizi zifuatazi ni hatua za kufuatalia ili kitendo hicho kifanyike ipaswavyo: Lowesha mikono yako katika maji safi ya bomba na kisha utumie sabuni; Sugua mikono yako pamoja ili kupata povu. Usisahau kusafisha kucha, vidole, pande zote za mkono na katikati mwa vidole vyako; Endelea kusugua kwa sekunde ishirini (20) hivi; Safisha mikono yako katika maji safi yanayotiririka; Kausha mikono yako kwa kutumia kitambaa safi au karatsi ya kukaushia mikono.

Kuhusu kucha, hakikisha kuwa zimekatwa ili viini vyta maradhi visije vikajificha chini ya kucha. Ni rahisi kufanya hivyo ili kuzuia magonjwa na kuokoa maisha yako.

Kuhusu usafi wa nywele, zinaweza kukatwa au kusukwa mara kwa mara na kusafishwa vizuri kwa kutumia maji na sabuni. Kitendo hiki kitasaidia katika kupunguza uyabisi na kuzuia chawa wa kichwani iwapo nywele zitakuwa chafu na kutooshwa vizuri.

Usafi wa mwili unahusiana sana na usafi wa nguo. Ni lazima wakati wowote nguo zetu ziwe safi yaani zifuliwe kwa sabuni na zibadilishwe mara kwa mara ili mtu asiwe na mwenendo wa kihuni.

Nguo zinazohusika ni: Mavazi ya nje kama vile shati, mpira, blauzi, kofia, kanzu, viatu, suruali...; Mavazi ya ndani kama vile chupi, soksi, sindiria,...; Mashuka kitandani na taulo. Soksi, taulo, mashuka au sindiria zikivaliwa kwa muda mrefu bila kubadilishwa hutoa harufu mbaya. Hivyo, chawa nao huweza kujitokeza na kuyahatarisha maisha yako.

Dumisha usafi wa mwili ili uweze kujilinda na maambukizi ya maradhi na kuepusha kuenea kwake. Kumbuka kuwa “Kinga ni bora kuliko tiba”.

1) Yataje mambo manne yanayoweza kuhusika na usafi. **(Alama 2)**

**Jibu:**

**Mambo manne yanayoweza kuhusika na usafi: - Mazingira yetu (kama vile usafi wa nyumba);**

- Vitu tunavyotumia katika kazi mbalimbali (kama vile usafi wa vyombo vya jikoni);**
- Lugha tunayotumia (kama vile usafi wa lugha au maneno);**

- **Roho zetu (kama vile usafi wa roho yaani kutakasa roho zetu kutokana na sala);**
- **Mwili wetu (Mfano: Usafi wa meno) na kadhalika.**

2) Je, ni upi umuhimu wa kumfunza mtoto kuhusu usafi wa mwili? **(Alama 3)**

**Jibu:**

**Kumfunza mtoto kuhusu usafi wa mwili ni jambo muhimu kwa sababu ni njia bora kabisa ya kumwepusha na maadhara mengi.**

3) “Baadhi ya watu hawana budi kutohusika na usafi wa mwili”.

Eleza waziwazi. **(Alama 2)**

**Jibu:**

**“Baadhi ya watu hawana budi kutohusika na usafi wa mwili”. Kauli hii ni ya uongo kwani kila mtu (awe mtoto au mkubwa, mtu mzima au mlemavu,... anahuksika na usafi wa mwili.**

4) Eleza tofauti baina ya “shule za chekechea” na “shule za msingi”. **(Alama 4)**

**Jibu:**

**“Shule za chekechea”: Ni shule za wale watoto wachanga ambao hawajafikia umri wa kuanza shule za msingi; “Shule za msingi” ni shule zinazotoa mafunzo ya kwanza ambayo ni kama nguzo ya elimu maishani mwetu.**

5) Kwa nini usafi wa kinywa ni muhimu sana? Eleza. **(Alama 3)**

**Jibu:**

**Usafi wa kinywa ni muhimu sana kwa sababu madhara yanayoweza kusababishwa na uchafu wa sehemu hizo ni mengi. Meno machafu huweza kuoza na kuvunjika, fizi inaweza kuvimba, kuoza na kutoa harufu mbaya na kadhalika.**

6) Ni wakati gani tunatakiwa kusugua meno? **(Alama 2)**

**Jibu:**

**Tunatakiwa kusugua meno mara kwa mara hasa hasa: Asubuhi tunapoamka kabla ya kifunguakinywa; - Kila mara baada ya chakula hasa vyakula vyenye sukari; - Usiku kabla ya kulala.**

7) Ni wakati gani tunalazimishwa kunawa mikono yetu? **(Alama 2)**

**Jibu:**

**Tunalazimishwa kunawa mikono yetu kwa ukawaida yaani:**

- Baada ya kutoka chooni;**
- Kabla ya kutayarisha, kuhudumia au kula chakula;**
- Baada ya kupiga chafya, kukohoa au kupenga kamasi;**
- Baada ya kutupa takataka;**
- Kabla na baada ya kumtembelea mgonjwa;**
- Baada ya kumgusa mnyama au kinyasi cha mnyama;**
- Baada ya kumbadilishia nepi mtoto au kumsaidia kutumia choo;**
- Kabla na baada ya kutibu jeraha au kidonda na kadhalika.**

8) Namna gani kitendo cha kuosha mikono kinafanyika? **(Alama 2)**

**Jibu:**

**Kitendo cha kuosha mikono kinafanyika namna hii:**

- Lowesha mikono yako katika maji safi ya bomba na kisha utumie sabuni;**

- **Sugua mikono yako pamoja ili kupata povu. Usisahau kusafisha kucha, vidole, pande zote za mkono na katikati mwa vidole vyako;**
- **Endelea kusugua kwa sekunde ishirini (20) hivi;**
- **Safisha mikono yako katika maji safi yanayotiririka;**
- **Kausha mikono yako kwa kutumia kitambaa safi au karatsi ya kukaushia mikono.**

9) Kwa nini ni lazima nguo za ndani za mtu ziwe safi? **(Alama 3)**

**Jibu:**

**Ni lazima nguo za ndani za mtu ziwe safi kwa sababu zikivaliwa kwa muda mrefu bila kubadilishwa hutoa harufu mbaya na hivyo, chawa nao huweza kujitokeza na kuyahatarisha maisha yake.**

10) Baada ya kusoma kisa hiki, fupisha habari nzima katika maneno 50.

**(Alama 4)**

**Jibu:**

**Msahihishaji achunguze kwamba mambo makuu au mawazo makuu yamezingatiwa katika ufupisho.**

11) Tumia maneno yafuatayo kutoka kisa cha habari ulichopewa, katika sentensi yenye maana. **(Alama 3)**

- a) meno
- b) mikono
- c) kucha

**Jibu:**

- a) Meno ya mama yanapendeza.**
- b) Si vizuri kula bila kunawa mikono.**

c) Kucha zako utazikata lini?

**SEHEMU YA II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama 30)**

12) Kamilisha ipaswavyo sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno uliyopewa: elimu, mikakati, uhaba. **(Alama 3)**

a) Ni lazima serikali yetu iunde ..... thabiti ya kufundisha fasihi simulizi shulenii.

b) Uvumbuzi wa maandishi ni mojawapo kati ya mambo yanayosababisha ..... wa kazi za fasihi simulizi.

c) Serikali ya Rwanda imepiga hatua kubwa katika kuendeleza ..... isiyo na ubaguzi.

**Jibu:**

**a) Ni lazima serikali yetu iunde mikakati thabiti ya kufundisha fasihi simulizi shulenii.**

**b) Uvumbuzi wa maandishi ni mojawapo kati ya mambo yanayosababisha uhaba wa kazi za fasihi simulizi.**

**c) Serikali ya Rwanda imepiga hatua kubwa katika kuendeleza elimu isiyo na ubaguzi.**

13) Tumia vitenzi vifuatavyo ujaze tungo za masharti zinazofuata ili ziwe na maana kamili: (**kuwa, kupata, kuchanjwa, kujenga, kujua**) **(Alama 5)**

a) ..... na pesa, ningenunua mbolea ili kurutubisha shamba langu na kupata mavuno mengi.

b) Nisingewafuga ng'ombe wengi, ..... maziwa ya kutosha.

ch) Ningalijua, ..... ili kujikinga na ugonjwa wa kifua kikuu.

d) Ningalikuwa na pesa, ..... nyuma ya kifahari Jijini Kigali.

e) ..... wakati anapopatikana, ningelikwenda kumwona daktari wa meno.

**Jibu:**

- a) **Ninge**kuwa na pesa, ningenuua mbolea ili kurutubisha shamba langu na kupata mavuno mengi.
- b) **Nisingemfuga ng'ombe, nisingepata maziwa ya kutosha.**
- c) **Ningalijua, ningalichanjwa ili kujikinga na ugonjwa wa kifua kikuu.**
- d) **Ningalikuwa na pesa, ningalijijengea nyuma ya kifahari Jijini Kigali.**
- e) **Ningelijua wakati anapopatikana, ningelikwenda kumwona daktari wa meno.**

**14)** Changanua tungo uliyopewa hapo chini kwa njia ya visanduku. **(Alama 3)**  
 a) Shangazi yangu na mjomba walisema ukweli.

**Jibu:**

SS					
KN				KT	
N	V	U	N	T	N
<b>shangazi</b>	<b>yangu</b>	<b>na</b>	<b>mjomba</b>	<b>walisema</b>	<b>ukweli</b>

**15)** Katika uandishi wa matangazo mambo mengi yanazingatiwa. Tumia NDIYO kwa jibu lililo sahihi na HAPANA kwa jibu lisilo sahihi. **(Alama 5)**

- a) Kuandika kichwa cha tangazo.
- b) Kumbukumbu namba (ikiwa unayo).
- c) Kutaja mtu au shirika linalotangaza.
- d) Salaam.
- e) Kuonyesha anwani ya mtoa tangazo.

**Jibu:**

- a) Kuandika kichwa cha tangazo: **NDIYO**
- b) Kumbukumbu namba (ikiwa unayo): **HAPANA**
- c) Kutaja mtu au shirika linalotangaza: **NDIYO**
- d) Salaam: **HAPANA**
- e) Kuonyesha anwani ya mtoa tangazo: **NDIYO**

**16)** Andika kwa upya sentensi zifuatazo kutokana na maelezo uliyopewa katika mabano. **(Alama 10)**

- a) Kabanda alirutubisha shamba ili kupata mavuno mengi. (Wakati ujao, hali yakinishi)
- b) Mariamu alisamehe watu wote waliopora mali yake. (Wakati uliopo, hali kanushi)
- c) Watu wengi hupenda kuomba Mungu kila siku. (Wakati uliopo, hali yakinishi)
- d) Kituo chetu kisingalilenga kutetea haki za watoto, kisingalipiga marufuku ubakaji wa watoto nchini mwetu. (Masharti, hali yakinishi)
- e) Usipomwadhibu mtoto, hatakuwa na nidhamu wala mwenendo bora. (Masharti, hali yakinishi)

**Jibu:**

- a) Kabanda atarutubisha shamba ili kupata mavuno mengi.**
- b) Mariamu hasamehe watu wote waliopora mali yake.**
- c) Watu wengi wanapenda kuomba Mungu kila siku.**
- d) Kituo chetu kingalilenga kutetea haki za watoto, kingalipiga marufuku ubakaji wa watoto nchini mwetu.**
- e) Ukimwadhibu mtoto, atakuwa na nidhamu na mwenendo bora.**

**17)** “Barua ni nusu ya kuonana. Thibitisha kauli hii. **(Alama 4)**

**Jibu:**

**Barua ni nusu ya kuonana. Hii ina maana kwamba unapoipokea barua kutoka kwa mtu fulani, ni kama kumwona mtu huyo lakini si kwa macho bali kuna kitu yaani barua kinachomwakilisha. Ni kusema kuwa mwandikiwa amemwona mwandishi katika barua yake au amemwona kwa nusu tu.**

### **SEHEMU YA III: FASIHI (Alama 25)**

18) Fasihi ina uhusiano wa karibu na lugha, na jamii ya watu. Thibitisha kauli hii. **(Alama 5)**

**Jibu:**

**Fasihi ina uhusiano wa karibu na lugha, na jamii ya watu kwa sababu hutumia lugha kwa kuwasilisha kazi zake. Na lugha hiyo ni lazima iwe chombo cha mawasiliano kati ya wanajamii wanayoielewa kwa urahisi.**

19) “Fasihi simulizi ya Kiswahili ilikuwepo kabla ya majilio ya wageni sehemu za pwani ya Bahari ya Hindi.” Fafanua kauli hii. **(Alama 5)**

**Jibu:**

**Ndiyo. Fasihi simulizi ya Kiswahili ilikuwepo kabla ya majilio ya wageni sehemu za pwani ya Bahari ya Hindi kwa sababu mahali hapo panajulikana kama makazi ya Waswahili. Hili linatokana na kuwa kuwepo kwa fasihi kunaenda sambaba na kuwepo kwa jamii husika ya watu.**

**20)** Chagua maana iliyo sawa inayofanana na methali zifuatazo: **(Alama 6)**

a) Dawa haitolewi bure: **Dunia si dunia ya vitu vya bure, Inafaa mtu afanye kazi.**

b) Chovya chovya humaliza buyu la asali.

ii) **Tunapotenga kitu kwa manufaa ya baadaye (akiba) na kuanza kukimega kidogo kidogo, mwisho tutashtuka tumekimaliza.**

c) Nguo za kuazima hazisitiri matako:

ii) **Usiwategemee wengine katika kukidhi mahitaji yako.**

**21)** Andika kwa mtindo wa kinathari wazo kuu linalozungumziwa katika ubeti wa kwanza wa shairi lifuatalo. **(Alama 5)**

### **ASIYESIKIA LA MKUU**

1. Ulevi kitu kibaya, sahibu na kueleza,

Utakuletea dhiya, kuonyesha miujiza,

Waja kukuona mbaya, na wao watakubeza,  
Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu.

2. Mwisho utafirisika, ponda malikufa kwaja,  
Huja we ukashituka, ukabakia kiwanja,  
Pesa zimekuponyoka, zikienda kwa wajanja,  
Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu.

**Jibu:**

**Ubeta huu unazungumzia ulevi kama kitu kibaya kinachoweza  
kumuaibisha mlevi na kumsumbuwa anapoendelea na tabia hiyo ya  
matumizi ya vileo. Watu wanaweza kumwona mbaya na kumdharaau kama  
hataki kurekebisha mwenendo huo mbaya.**

22) Kuna mafunzo na maadili yanayofuatiliwa na jamii kutoka hadithi ya fasihi  
simulizi. Thibitisha kauli hii. **(Alama 4)**

**Jibu:**

**Mtu anaweza kuwa na tabia mbaya lakini baada ya kuisikiliza hadithi  
akabadili tabia zake mbaya. Kuna tabia mbaya za kuepukana nazo kama  
vile ulevi, uzembe, uasherati, wizi, udanganyifu, uovu, chuki, uoga, na  
kadhalika.**

**Kwa upande mwingine, kuna pia tabia nzuri za kufuatiliwa kama vile wema,  
ukarimu, upendo, ushirikiano, na kadhalika.**

**SEHEMU YA IV: UTUNGAJI**

**(Alama 15)**

23) Chagua mada moja kati ya hizi zifuatazo kisha utunge insha yenyе maneno  
150.

a) Maneno matamu humtoa nyoka pangoni.

**Jibu:**

**Baadhi ya hoja:**

- a) Kuongea na mtu kwa adabu, staha, maneno mazuri huwavutia watu na kutamani kukusikiliza.
  - b) Maneno mazuri huwashawishi watu kukusikiliza na kukubaliana na unachokisema.
  - c) Unaweza kupata vitu vingine vizuri kutoka kwa watu kwa tabia ya kuwa na kauli nzuri.
- b) John alipigwa marufuku shulenii.

**Jibu:**

**Baadhi ya hoja:**

- a) Kueleza maana ya nahau inayopatikana katika kichwa cha insha.
- b) Kuonyesha sababu mbalimbali zilizomfanya John afukuzwe shulenii kama vile: kuwa na kiburi, kuendeleza ulevi, kutoroka shule wakati wa masomo, kuiba vifaa vya wenzake, kuleta vyakula na vinywaji visivyokubalika, kufanya uzinzi, na kadhalika.
- c) Kufupisha mambo yaliyosemwa katika kiini na kuwaonya wanafunzi wengine kutofuata mienendo mibaya ya John.

#### **Mwongozo wa kukosoa insha (Alama 15)**

**FANI**

- Kichwa/ Mada: (**alama 2**)
- Urefu wa insha: (**alama 1**)
- Pembezo: (**alama 1**)
- Usafi: (**alama 1**)

**MAUDHUI**

- Utangulizi: (**alama 1**)
- Mwili: Maelezo ya hoja angalau tatu (**alama 7**): Sarufi na matumizi ya lugha: (**alama 1**) (makosa mawili ni kutoa alama 0.5; makosa manne ni kutoa alama 1)
- Hitimisho: (**alama 2**)

**Mwisho.**